



NATIONAL HEALTH INSURANCE FUND

**MUONGOZO MPYA WA TELE KWA TELE WA KUZILIPA
HALMASHAURI ZINAZOTEKELEZA MPANGO WA MFUKO WA
AFYA YA JAMII (CHF/TIKA)**



JUNE, 2015

MUONGOZO WA TELE KWA TELE

N.	ENEEO	MAMBO YA KUZINGATIA
1	Barua ya maombi ya tele kwa tele kutoka Halmashauri.	<p>Barua ya maombi ya tele kwa tele itakayosainiwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri au anayekaimu nafasi hiyo.</p> <p>Barua hiyo pamoja na mambo mengine.</p> <ul style="list-style-type: none"> • ieleze kiasi kinachoombwa , • idadi ya wanachama, • kipindi cha maombi • viambatanisho muhimu vilivyopo katika maombi hayo • Igongwe muhuri wa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri. <p>Barua hiyo ioneshe mgawanyo wa asilimia ya matumizi ya fedha zilizotumika kununulia dawa hadi kufikia kipindi cha maombi.</p>
2	Fomu ya Maombi ya Tele kwa Tele (Matching fund application form)	<p>Fomu ya maombi ya madai ya Tele kwa Tele itawasilishwa kwa mujibu wa mfano wa fomu iliyoambatanishwa. Katika fomu hiyo ieleze mwaandaaji wa madai, kukaguliwa kwa madai na Mganga Mkuu wa Halmashauri na kuidhinishwa na Mkurugenzi wa Halmashauri. Fomu isomeke kama ifuatavyo;</p> <ul style="list-style-type: none"> • Kaya /mwanachama mpya. • Kaya / Wanachama za/wa zamani • Mchango wa kaya/mwanachama • Fomu ioneshe tarehe, cheo na namba ya simu • Fomu igongwe muhuri wa Halmashari.
3	Taarifa ya Mapato ya CHF/TIKA katika jedwali	<p>Taarifa hii pamoja na mambo mengine Upande wa Mapato uonyeshe</p> <ul style="list-style-type: none"> • Jina la kata na kituo cha kutolea huduma, • Idadi ya wanachama waliojiunga na CHF/TIKA • Michango ya wanachama wa CHF/TIKA • Stakabadhi namba za michango ya CHF/TIKA • Malipo ya Tele kwa Tele awamu iliyopita • Michango ya NHIF • Papo kwa papo • Mapato mengineyo • Jumla ya mapato

4	Taarifa za hesabu za kibenki (bank statement)	Taarifa hizi ziwe za kipindi chote cha maombi na iainishe fedha zote zinazoombewa Tele kwa Tele zilizo kwenye taarifa ya kibenki (Bank statement).
5	Nakala za stakabadhi za Halmashuri	Itatakiwa kuambatanisha nakala halisi ya; <ul style="list-style-type: none"> • Stakabadhi ya malipo ya serikali (Government exchequer receipts) au • Stakabadhi ya malipo ya Halmashuri kwa ajili ya kukiri kupokelewa fedha za CHF/TIKA kutoka katika vituo vya afya vya uchangiaji au • Kama stakabadhi zitatolewa vivuli, vivuli vya stakabadhi hivyo vithibitishwe kwa kugongwa muhuli wa uhalisia (Certified receipts of the true copy of the original) NB: Jumla ya fedha za CHF zilizoainishwa kwenye stakabadhi zinatakiwa kuendana na michango inayoombwa.
6	Viambatanishi kwa waombaji wapya	Iambatanishwe nakala ya sheria ndogo ya Halmashuri zilizosainiwa na Waziri mwenye dhamana kwa waombaji wapya.
7	Orodha ya wanachama wachangiaji	Iambatanishwe orodha inayoonyeshe idadi na majina ya wanachama wachangiaji wote wanaoombewa fedha za tele kwa tele kwa kipindi cha maombi. Jambo la kuzingatia; idadi ya majina ya wanachama wachangiaji wanaoombewa tele kwa tele na fedha iliokusanywa benki na zilizokwenye stakabadhi ifanane/kifanane na kiasi kinachoombwa katika madai hayo.
8	Kiwango cha chini cha maombi ya Tele kwa Tele	Halmashuri iombe fedha za Tele kwa Tele zisizopungua 5,000,000/- . Baada ya kukusanya fedha za michango ya wanachama wa CHF/IKA bila ya kuchanganywa na fedha za papo kwa papo katika stakabadhi zitakazo ambatanishwa. Aidha, Halmashuri zitalazimika kuomba kwa kiwango cha fedha tajwa hapo juu au kila robo mwaka hata kama kiwango walichokusanya hakijafikia milioni tano (5,000,000/-) .
9	Namna ya Kuwasilisha Madai	Maombi ya Tele kwa Tele yanatakiwa kupitia ofisi za Mikoa za Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya ili yahakikiwe kwanza kabla ya kuwasilishwa makao makuu. waratibu walete madai NHIF kabla ya siku 30 kuisha baada tu ya robo mwaka. NHIF inatakiwa kulipa madai hayo ndani ya siku 30.
10	Vigezo Kuzingatiwa	Madai yatatakiwa kukidhi viambatanisho tajwa hapo juu na yale ambayo hayatakidhi yatasimamishwa hadi pale yatakapokidhi vigezo vya malipo.

Mfano wa fomu ya Maombi ya Tele kwa Tele na Taarifa ya Mapato ya Mfuko wa Afya ya Jamii kwa kipindi cha maombi zimeambatanishwa kama kiambatanisho na 1 & 2.

HALMASHAURI YA.....
FOMU YA MAOMBI YA TELE KWA TELE

TAREHE YA MAOMBI:

KIASI KINACHOOMBWA:

KIPINDI CHA MAOMBI:

KIPINDI CHA MAOMBI YA MWISHO KUFANYIKA:

IDADI YA WANACHAMA WA TIKA:

IDADI YA KAYA KWENYE MAOMBI:

- KAYA MPYA:
- KAYA ZA ZAMANI:
- WANAFUNZI:

ADA YA MWACHAMA:

MADAI YAMEANDALIWA NA MRATIBU WA CHF:

JINA:

SAHIHI:

TAREHE

MADAI YAMEKAGULIWA NA MGANGA MKUU:

JINA:

SAHIHI:

TAREHE

MADAI YAMEIDHINISHWA NA MKURUGENZI MTENDAJI WA WILAYA:

JINA:

SAHIHI:

TAREHE

HALMASHAURI YA WILAYA YAIDARA YA AFYAMCHANGANUO WA MAPATO YA FEDHA ZA UCHANGIAJI ZA MFUKO WA AFYA YA JAMII (CHF)KIPINDI CHAHADIMAPATO

S/N	KATA	VITUO VYA HUDUMA	IDADI YA KAYA (SENSA YA 2012)	IDADI YA WATU (SENSA 2012)	IDADI YA KAYA ZILIZOJIUNGA UANACHAMA WA CHF	MICHANGO YA UANACHAMA TSHS	RISITI NA.YA MICHANGO YA CHF	PAPO KWA PAPO	NHIF	MENGIN EYO (KfW)	JUMLA YA MAPATO
JUMLA											